

Maswali

1. Nani alinunua Yusufu kutoka kwa wafanya biashara?
2. Mbona Yusufu aliwekwa gerezani?
3. Wafungwa gani walikuwa na ndoto usiku moja?
4. Mnyweshaji aliota eti nini?
5. Ndoto yake ilimaanisha nini?
6. Mwokaji aliota eti nini?
7. Ndoto yake ilimaanisha nini?
8. Farao aliota eti nini?
9. Ndoto yake ilimaanisha nini?
10. Nani alifanywa mtawala wa Misri? Alifanya nini?

Majibu

1. Potifa alimnunua.
2. Mke wa Potifa alisema uongo juu ya Yusufu.
3. Mnyweshaji na mwokaji.
4. Aliona mzabibu na matawi matatu. Huo mzabibu ulikua vizuri ukaweka mizabibu mizuri. Alikamua hizo mizabibu kwa kikombe cha Farao na akampa.
5. Baada ya siku 3 atatolewa gerezani na aende kuwa mnyweshaji wa Farao tena.
6. Alikuwa na vikapu 3 vya mikate kichwani. Ndege zilizikula.
7. Baada ya siku 3 atauawa
8. Ng'ombe 7 waliokonda walikula ng'ombe 7 walionona na hawakunona. Masuke ya nafaka 7 membamba yalikula masuke ya nafaka 7 manono
9. Kutakuwa na miaka 7 ya mavuno mazuri baadaye miaka 7 ya njaa.
10. Yusufu alinywa mtawala wa Misri. Aliweka nafaka nydingi wakati wa mavuno mazuri.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



10 Yusufu kule Misri

Marejeo

Mwanzo mlango wa 39, 40 na 41

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yusufu aliamini Mungu katika shida zake zote za maisha yake. Mungu alitumia maisha ya Yusufu kutimiza kuzudi lake.

Maneno maalum

- 10.1 Potifa + nunua Yusufu + simamia + mke wa potifa +uongo + gereza
- 10.2 Mlinzi wa gereza + Yusufu +simamia + mnyweshaji + mwokaji + ndoto
- 10.3 Mnyweshaji + divai + matawi 3 + mizabibu + kikombe cha Farao + siku 3 + mnyweshaji tena + nikumbuke
- 10.4 Mwokaji + vikapu 3 vya mikate + ndege + siku 3 + kufa
- 10.5 Farao + ndoto mbili + Yusufu + ng'ombe 7 wanono + ng'ombe 7 wamekonda + masuke manono 7 ya nafaka + masuke membambe 7 ya nafaka + miaka 7 mavuno mazuri + miaka 7 njaa
- 10.6 Mtu wa hekima + Yusufu + mtawala + kusanya chakula + weka

10.1 Potifa nahodha wa askari wa Farao alinunua Yusufu kutoka kwa wafanyi biashara. Potifa alipenda Yusufu. Alimweka kusimamia kila kitu kwa nyumba yake. Yusufu aliangalilia Potifa kila kitu.

Mke wa Yusufu alisema uonga juu ya Yusufu. Alidanganya kwamba, "Alinishambulia." Potifa aliamini mkewe. Yusufu aliwekwa kwa gereza yenye wafungwa wa Farao walifungwa.


10.2 Mlinzi wa gereza alipenda Yusufu. Alimweka kusimamia wafungwa wengine. Mnyweshaji wa Farao na mwokaji waliletwa kwa hiyo gereza. Usiku moja, wote wawlili waliota ndoto. Yusufu aliwaliza, "Niambia hizo ndoto?"



10.3 Mnyweshaji wa Farao alimwambia, "Niliona mzabibu na ulikuwa na matawi matatu. Ulikua vizuri na ukaweka mizabibu mibivu nzuri. Kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu. Nilikamua hizo mizabibu kwa kile kikombe na nikapea Farao?"



Yusufu alimwambia, "Baada ya siku tatu, utakuwa mnyweshaji wa Farao tena na utamwakia divai. Tafadhali nikumbuke na uambia Farao anitoe gerezani. Mimi sikufanya kosa lolote."



10.4 Mwokaji alisema ndoto yake. "Nilikuwa na vikapu vitatu vya mikate juu ya kichwa changu, na ndege walikuja wakizikula." Yusufu alimwambia, "Baada ya siku tatu utauawa." Ilifanyika vile Yusufu alisema. Lakini mwokaji alisahau yote kuhuzu Yusufu.

10.5 Siku moja Farao alikuwa na ndoto mbili. Ilipofika asubuhi aliiita waganga wote wa Misri. Aliwaliza wamwambia maana ya ndoto zake. Lakini hakukuwa hata mmoja aliyejua maana. Halafu mnyweshaji alikumbuka Yusufu. Alimwambia Farao juu ya Yusufu.

Yusufu aliletwa kwa Farao. Farao akamwambia, "Nilikuwa na ndoto mbili. Niliona ng'ombe saba wanono wakatoka nje ya mto. Halafu ng'ombe waliokonda nao walitoka. Wale waliokonda walikula walionona. Lakini hawakukuwa wanono.

Baadaye niliona masuke ya nafaka saba wakikua wanono na wakawa wazuri. Halafu kukatokea masuke ya nafaka saba yalikuwa dhaifu na yamekonda. Yaliyokonda saba yalikula yale masuke saba yaliyonona."

Yusufu aliambia Farao, "Ndoto zako zote mbili zinamaana moja. Mungu amekwambia chenyе atafanya. Ng'ombe saba wanono na masuke ya nafaka saba nzuri ni miaka saba ya mavuno nyingi. Ng'ombe waliokonda saba na masuke ya nafaka saba dhaifu ni miaka saba ya njaa. Kutakuwa na miaka saba ya mavuno mengi na miaka saba ya njaa."

10.6 Farao aliuliza Yusufu, "Nifanye nini?" Yusufu alimwambia, "Lazima uchague mtu aliye na hekima na asimamie nchi." Farao alisema, "Ni nani anaweza kuwa na hekima kuliko Yusufu?" Kwa hivyo Farao alimfanya Yusufu kuwa mtawala wa nchi ya Misri.

Farao alichukuwa pete yake yenye muhuri na akaiweka kwa mkono wa Yusufu. Alimpa nguo za heshima tena akamwekeea mkufu wa dhahabu kwa shingo. Wakati wa mavuno mengi Yusufu alichukua chakula kingi na kuweka maghala kwa za miji.